# SERA BUNGE NA URATIBU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA
40412 DODOMA TANZANIA.

2025


zika
MACHO





# WAZIRI MKUU MAJALIWA ATOA WITO WADAU KUIMARISHA USHIRIKIANO NA SERIKALI

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ametoa wito kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi na taasisi za dini kuimairisha ushirikiano na Serikali na kujiunga katika mtandao wa kitaifa wa usimamizi wa huduma za kibinadamu.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Willium Lukuvi wakati akimwakilisha Waziri Mkuu katika Maadhimisho ya Siku ya Watoa Huduma za Misaada ya Kibinadamu Duniani tarehe 19 Agosti, 2025 Jijini Dodoma.

“Ninatoa wito kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi na taasisi za dini kuimairisha ushirikiano na Serikali na kujiunga katika mtandao wa kitaifa wa usimamizi wa huduma za kibinadamu, kwa kufanya hivyo kutaongeza uratibu, uwajibikaji na ufanisi katika kushughulikia majanga” ameeleza

Aidha, amesisitiza watoa huduma za kibinadamu kutia mkazo katika suala la kuelimisha umma ili wananchi waweze kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu ili kuweza kupunguza athari za majanga pindi yanapotokea.

“Kwa kuwa yapo majanga ambayo hayakwepeki, ninawasihi sana watoa huduma za kibinadamu, kutilia mkazo suala la kuelimisha umma. Wananchi waelimishwe kuzingatia maelekezo yanayotolewa na watalaamu ili kupunguza athari za majanga yanapotokea” amefafanua.













# WAZIRI LUKUVI ATOA MAAGIZO YA RAIS SAMIA AJALI YA MGODI NYANDOLWA

Waziri wa nchi Ofisi ya waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge William Lukuvi akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa maagizo kwa viongozi wa Serikali waliopo maeneo ya ajali ya mgodini kushiriki taratibu zote za mazishi kwa walifariki ajali ya mgodini na kuwakilisha rambirambi zake kwa wahusika huku akisihii kuendelea kuratibu vyema shughuli ya uokoaji inayoendelea.

Ameyasema hayo wakati wa kikao na viongozi pamoja na ndugu wa waathirika wa ajali ya mgodini katika eneo la tukio la ajali ya mgodi unaomilikiwa na Kikundi cha Wachapakazi katika machimbo ya Nyandolwa Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga.

“Rais Samia kaniagiza kuwafikishia salamu za pole na rambirambi pia kanituma kuleta maagizo kwa viongozi wa serikali waliopo eneo hili kuhakikisha wanahudhuria misiba yote ya watu waliopoteza maisha katika ajali hii na kuwakilisha rambirambi alizotoa katika familia hizo” amesema Lukuvi.



# UZINDUZI WA MFUMO WA ANUANI ZA MAKAZI ZANZIBAR WAFANA

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Ummy Nderiananga, ameshiriki katika hafla ya uzinduzi wa mfumo wa anuani za makazi, unaolenga kutoa huduma ya barua ya utambulisho wa mkazi kwa njia ya kidijitali.

Uzinduzi huo umefanyika leo katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar, ukiongozwa na Mgeni Rasmi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Ummy amepongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa jitihada zao za kuimarisha huduma za kijamii kupitia mifumo ya kidijitali.




"Niwapongeze kwa kuendelea kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa urahisi zaidi kupitia teknolojia. Mfumo huu utarahisisha utambuzi wa makazi na uboreshaji wa utoaji wa huduma mbalimbali serikalini," alisema Mhe. Ummy.

Aidha, amezipongeza wizara zote za kisekta kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano wao uliowezesha utekelezaji wa mfumo huo muhimu kwa maendeleo ya Taifa









# MAKATIBU WAKUU WATETA MIKAKATI YA KUENDELEZA SAFARI CHANNEL YA TBC



Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. James Kilabuko, ameongoza kikao cha Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali kilichofanyika leo jijini Dodoma kwa lengo la kujadili namna bora ya kuimarisha uendeshaji wa Tanzania Safari Channel chini ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Kilabuko amesema chaneli hiyo imekuwa nyenzo muhimu ya kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia vivutio vya utalii vilivyopo nchini, hivyo ni muhimu kwa taasisi zote za serikali kushirikiana katika kuiendeleza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Dkt. Ayub Rioba Chacha, akiwasilisha taarifa kuhusu chaneli hiyo, ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusaini sheria mpya ya TBC, ambayo imefungua milango ya maboresho ya kiutendaji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma.

Chaneli ya Tanzania Safari Channel imekuwa chombo mahsusi cha kuitangaza Tanzania kama nchi yenye vivutio vya kipekee duniani, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kimkakati kukuza sekta ya utalii.








# SERIKALI YAFUNGUA MILANGO YA FURSA, KWA WAKULIMA WA MWANI

Serikali imewataka wakulima wa mwani nchini kutumia mbinu bora na za kisasa za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kuongeza ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Hayo, yamebainishwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, Dkt. James Kilabuko wakati akifunga mafunzo ya kujenga uwezo kwa vikundi vinavyojihusisha na kilimo cha mwani yaliyofanyika Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga kwa muda wa siku kumi na mbili kuanzia tarehe 04 hadi 15 Agosti,2025.

“Mafunzo mliyojifunza ya kilimo bora cha mwani yatawasaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji na ubora wa mwani katika soko la ndani na nje ya nchi,” alisema na kuongeza kuwa, “Mafunzo ya uongezaji thamani, matumizi bora ya kemikali mnazotumia kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na mwani, vifungashio vya bidhaa, zitazoweza kuwatambulisha na kuzitangaza bidhaa zenu ndani na hata nje ya nchi, upatikanaji wa masoko ya mwani” Alisema Dkt. Kilabuko.

Pia Dkt. Kilabuko alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima wa mwani ili kuongezea mnyororo wa thamani wa zao hilo nchini.

Vilevile, aliwataka wakulima hao kujipangia utaratibu wa kufikisha maarifa waliyoyapata kwa wanakikundi wengine ambao hawakupata fursa ya kupata mafunzo hayo kwa kufanya mazoezi katika vikundi vyao hususani mafunzo ya wokozi na huduma ya kwanza majini.



# SERIKALI YA SISTIZA USHIRIKIANO NA SEKTA BINAFSI KATIKA UTEKELEZAJI WA ASDP II

Serikali imesisitiza umuhimu wa ushirikiano wa karibu kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), hususan katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu.

Akizungumza katika kikao kazi cha waratibu wa programu hiyo kilichofanyika leo Agosti 27, 2025 jijini Dodoma, Mratibu wa Taifa wa ASDP II kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, Dkt. Salim Nandonde, alisema sekta binafsi ni nguzo muhimu katika mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo na mifumo ya chakula nchini.

“Uratibu wa ASDP II unaoratibiwa katika ngazi ya taifa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na OR-TAMISEMI katika ngazi za mikoa na halmashauri, unalenga kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu, hasa kwenye kuongeza thamani katika mazao na mifumo ya chakula ili kuongeza tija na ushindani,” alisema Dkt. Nandonde.












# ZANZIBAR YACHOTA UZOEFU DODOMA: YAJIANDAA KUJENGA MJI WA SERIKALI KISAKASAKA

Kamati ya wataalamu kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Ikiingozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar Dkt. Islam Seif Salum imetembelea miradi mikubwa jijini Dodoma ikiwemo Mji wa Serikali Mtumba na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, kujifunza utekelezaji wa Ujenzi wa Mji wa Serikali.

Ziara hiyo inalenga kuandaa mazingira ya ujenzi wa ofisi za Serikali na Baraza la Wawakilishi eneo la Kisakasaka, Zanzibar.

Viongozi hao wamempongeza Rais Dkt. Samia kwa kuimarisha maendeleo ya Makao Makuu ya Nchi kupitia miradi ya kimkakati.

## MHARIRI

Everline Mkokoi


## WAANDISHI / WAPIGA PICHA

Beatrice Lyimo
Fredy Kabutu
Nyamagori Kitwana
Devota Songorwa
Silvanus Mauki
Tumaini Mnunge
Tegemeo Kastus

## MSANIFU WA JARIDA

Muhsin Othman
Tegemeo Kastus



Jarida hili hutolewa na:
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu
Pakua jarida hili kupitia:
www.pmo.go.tz